HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30/6/2017

Mh. Mwenyekiti,
Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
Hiki ni kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha kujadili taarifa mbalimbali za Fedha, Uongozi na Mipango. Kikao hiki kinafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa agizo namba 21.Kwa msingi huo ni jukumu la kila mjumbe kupitia taarifa hii na kuchangia maoni ambayo yataisaidia Halmashauri kufikia lengo kuu la kutoa Huduma nzuri na endelevu zenye kuleta Maendeleo katika Wilaya yetu ya Mufindi.

1) Mapitio ya Bajeti 2016/17
A) Mapato

Mh. Mwenyekiti,
Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilipitisha bajeti ya kukusanya na kupokea jumla ya Tshs.**50,638,039,096.67** Makusanyo haya yamegawanyika kama ifuatavyo;

Na.	Maelezo	Kiasi
1.	Mapato ya ndani	3,855,915,000.00
2.	Ruzuku Mishahara	34,971,890,400.00
3.	Ruzuku matumizi ya kawaida	2,603,879,000
4.	Wadau wengineo	9,206,354,696.67
JUMLA		**50,638,039,096.67**

Aidha kwa mwaka wa fedha 2016/17, Halmashauri imeanza na bakaa yaTshs. **1,847,315,416.81** Fedha hizi zimegawanyika kama ifuatavyo;

Jina la akaunti	Namba ya akaunti	Kiasi
Matumizi ya kawaida	60210001175	199,088,540.99
Miradi ya Maendeleo	60210001176	595,005,989.24
Barabara	60210001178	558,547,060.67
Maji	60210004850	162,082,290.60

Mapato ya ndani	60210001172	92,243,670.91
Akaunti ya Mishahara	60210001174	125,210,237.09
Elimu	60210018989	2,980,055.31
Afya	60210018991	112,157,572.00
Jumla		**1,847,315,416,.81**

Katika kipindi cha kuishia May 2017 Halmashauri kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeongezewa bajeti kwenye mfumo funganifu wa malipo katika vifungu vya Mradi wa TASAF na Kihansi nje ya bajeti ya mwaka ,ambapo **Tshs 1,030,719,225.24** imeongezeka katika mradi wa TASAF na **Tshs 40,132,260.00** katika mradi wa Kihansi.Aidha Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs 73,325,000.00** kutoka UNICEF nje ya makisio na hivyo kufanya jumla ya ongezeko la makisio ya **Tshs 1,144,176,485.24,** na kwa mwezi June 2017 Halmashauri imepokea fedha kiasi cha **Tshs 363,919,904.00** kutoka Unicef nje ya makisio.

Mh. Mwenyekiti,

Ukijumlisha fedha ya bakaa, makisio yaliyokuwa yameidhinishwa, bajeti ya Halmashauri kwa Mwaka 2016/2017 inakuwa na jumla ya Tshs.**53,629,530,998.72** kwa mchanganuo ufuatao;

Chanzo cha Mapato	**Kiasi**
Mapato ya ndani	3,948,158,670.91
Ruzuku ya Mishahara	35,097,100,637.09
Matumizi mengineyo	2,918,105,168.30
Miradi ya Maendeleo	11,666,166,522.42
Jumla	**53,629,530,998.72**

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti

Katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Halmashauri ya wilaya ya Mufindi inategemea kutumia jumla ya Tshs.**53,629,530,998.72** Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo;

Chanzo cha Matumizi	**Kiasi**
Mishahara	35,097,100,637.09
Matumizi mengineyo	6,866,263,839.21
Miradi ya maendeleo	11,666,166,522.42
Jumla	**53,629,530,998.72**

2) Hali Halisi

A) Mapato

Mh. Mwenyekiti,

Katika kipindi cha Julai hadi June 2017, Halmashauri ilikusanya na kupokea jumla ya Tshs. **41,424,567,785.68** Kati ya Mapato haya Tshs **3,233,548,976.11** ni mapato yaliyotokana na vyanzo vya ndani,Tshs **29,486,614,690.32** ni Mishahara,Tshs **6,275,128,120.25** ni Miradi ya maendeleo na **Tshs 2,429,276,000** ni fedha za matumizi ya kawaida.

Mlinganisho wa Mapato halisi ya Tshs **41,424,567,785.68** kwa kipindi cha Julai hadi June 2017 na makisio ya Tshs **51,782,215,581.91** inaonesha kuwa Halmashauri imekusanya asilimia **79.89** ya lengo la mwaka wa fedha wa 2016/17.Aidha mlinganisho wa mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai 2016 – June 2017 ya Tshs **3,233,548,976.11** na Makisio ya mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani ya Tshs **3,855,915,000.00** kwa kipindi hicho hicho, yanaonesha kuwa Halmashauri imekusanya asilimia **83.86** ya lengo la mwaka .

Mh Mwenyekiti,

Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha Julai – June 2017 unaonesha kuwa hali ya ukusanyaji wa mapato haikuwa ya kuridhisha . Hali hii inasababishwa na

- Kurejeshwa kwa kiasi kidogo cha kodi ya ardhi kwa mwaka huu.Hadi June 2016 jumla ya shs 12,050,870.78 zilikuwa zimerejeshwa kati ya shs 128,698,000
- Chanzo cha ushuru wa stendi kutoanza kukusanywa kutokana na kutokamilika kwa ujenzi.
- Ushuru wa chai kupungua kutokana na kuchelewa kwa mvua za masika na hivyo kupunguza uzalishaji wake
- Mchakato wa uuzaji wa viwanja kama ilivyo katika bajeti kutokamilika katika mwaka huu wa fedha.
- Mwitikio mdogo wa jamii katika uchangiaji wa huduma za Afya – CHF
- Miundombinu ya barabara kutokuwa mizuri
- Kutokuwepo kwa Gari maalumu kwa ajili ya ufuatiliaji wa Mapato

Ili kukabiliana na changamoto hizi kwa mwaka wa fedha wa 2017/18 Halmashauri imejipanga kufanya yafuatayo;

- Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kwa kuiwezesha timu ya ufuatilaji wa mapato kufanya ukaguzi na doria mara kwa mara katika maeneo yanayokusanywa mapato na njia zinazotumika kutorosha mapato
- Kuendeleza mchakato wa Ujenzi wa stendi ya Nyololo na Igowole ili tuweze kukusanya ushuru.

- Kuendelea kutambua na kufuatiliaji kampuni zote zinazofanya biashara katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi
- Kufuatilia na kukusanya mapato yaliyoainishwa katika mabadiliko ya sheria ndogo zilizopelekwa TAMISEMI kama vile ushuru wa madini na hewa ya ukaa
- Kuhimiza uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo
- Kushirikisha wadau wengineo wa maendeleo katika kuanzisha miradi mikubwa ya uwekezaji kama ya Umeme n.k
- Kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kuchangia mfuko wa bima ya Afya
- Kuendelea kutumia njia ya Ki electronic ya kukusanyia mapato kwa kununua POS 30

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti,

Matumizi hutegemea mapato yanayokusanywa. Kwa kipindi Julai - June 2017, Halmashauri imetumia jumla ya **Tshs.41,771,669,019.05** Matumizi haya yamegawanyika kama ifuatavyo;

Chanzo cha Matumizi	**Matumizi halisi.**
Mishahara	29,486,614,690.32
Matumizi mengineyo	5,418,388,870.92
Miradi ya Maendeleo	6,866,665,457.81
Jumla	**41,771,669,019.05**

3) Taarifa Nyinginezo

a) Usuluhisho wa Benki

Mh. Mwenyekiti,

Usuluhisho wa benki kwa mwezi June 2017 umefanyika kwa akaunti zote tisa zifuatazo:

Na	Jina la Akaunti	Salio Benki	Salio Halmashauri
1	Mishahara (60210001174)	118,408,893.96	114,890,860.10
2	Miradi ya Maendeleo (60210001176)	994,122,127.96	580,915,991.91
3	Mfuko wa Barabara (60210001178	785,373,834.54	532,196,173.54
4	Mradi wa Maji (60210004850)	68,100,201.49	37,852,754.29
5	Afya (60210018991)	163,900,983.90	41,128,003.90
6	Elimu (60210018989)	2,170,106.71	195,880.31
7	Other Charges (60210001175)	90,638,157.52	9,612,953.88
8	Deposit (60210001177)	543,212,874.44	115,547,815.15
9	Own Source (60210001172)	183,421,565.51	183,421,565.51

b) Akaunti ya Amana

Akaunti ya Amana huweka amana mbalimbali. Wakati tunaanza mwaka huu wa fedha (1/7/2016) mfuko huu ulianza na salio anzia la Tshs. **254,504,044.71**. Mapato kwa mwezi Julai – June 2017 yalikuwa Tshs **1,307,954,833.88** na hivyo kuifanya Akaunti hii kuwa na jumla ya Tshs **1,62,458,878.59** ilipofika tarehe 30/6/2017. Aidha Matumizi kwa Mwezi Julai – June 2017 ni Kiasi cha Tshs **1,446,911,063.44** na hivyo kufanya Akaunti hii kuwa na bakaa ya Tshs **115,547,815.15**

c) Madeni

Mh. Mwenyekiti,

Wakati tunaanza mwaka huu wa Fedha (2016/17), Halmashauri ilikuwa na deni ya Tshs**.1,081,421,695.83** kati ya deni hili Shs **28,890,152.00** ni deni la kandarasi za Barabara na Shs **1,056,531,543.83** ni deni la huduma na vifaa mbalimbali. Hadi tarehe 30/6/2017 jumla ya deni lenye thamani ya **Tshs 485,279,068.19** ilikuwa limelipwa na hivyo Halmashauri kubakia na deni la **Tshs 596,142,627.64**

Mh. Mwenyekiti,

Pamoja na Taarifa hii nimefungasha Jedwali Mbalimbali zinazoonesha mwenendo wa mapato na matumizi katika kipindi hiki pamoja na jedwali la wadai wa Halmashauri.

Mh. Mwenyekiti,

Naomba Kuwasilisha.

Felisi B. Mhando
KNY: MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
MUFINDI